MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR

S.L.P. 3650
VICTORIA GARDEN
ZANZIBAR

SIMU: 024 2232916
MOB: 0774 824 242
FAX: 024 2231461

# MUONGOZO WA TUNZO YA WAANDISHI WA HABARI (ZAECA JOUNALIST AWARD 2020/21)

## UTANGULIZI

Tasnia ya habari ni muhimili usio rasmin wenye nguvu kubwa ya kuelimisha umma na kukemea maovu ili kujenga jamii yenye kufuata maadili hususan katika kutokomeza vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi. Kutokana na umuhimu huo, ZAECA inalazimika kuendelea kushirikiana na wanahabari ili kufanikisha shughuli zake za kila siku. Katika kufanyia kazi azma hii kwa vitendo, Mamlaka inaendelea na utaratibu wake wa kuitisha na kuendesha tunzo ya waandishi wa habari. Mbinu hii itatoa fursa kwa vyombo vya habari kuelimisha umma na kusaidia kubaini matukio ya uhalifu ikiwa ni sehemu ya ushiriki wa shindano hili.

Kutokana na nchi ya Tanzania kuingia katika uchaguzi Mkuu mwaka 2020, ZAECA kwa kushirikiana na washirika wake wengine wa tunzo hii, wameamua kuendesha shindano hili chini ya kauli mbiu isemayo *“Kutojihusisha na Vitendo vya Rushwa katika Uchaguzi Huleta Matokeo Chanya +”.* Kauli hii itawapa uwanja mzuri wahabari kuuelimisha umma juu ya madhara ya rushwa katika uchaguzi na umuhimu wa kutojihusisha na vitendo vya rushwa ili kupata matokeo mazuri ya uchaguzi pamoja na kufichua jinai za rushwa zitakazojitokeza kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

**DHAMIRA MASHIINDANO**

Uratibu na uanzishaji wa tunzo hii umetokana na dhamira na madhumuni yafuatayo;

1. Kushajihisha uwajibikaji wa wanahabari na vyombo vya habari katika kuzuia vitendo vya rushwa kwa kuwaelimisha wananchi katika uchaguzi wa mwaka 2020.
2. Mashindano yanatarajiwa kuwa ni nyenzo ya kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa kudhihirisha makosa ya rushwa yatakayojitokeza katika uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.
3. Kupitia uendeshaji wa tunzo hii, kasi ya utendaji wa ZAECA itaongezeka kutokana na vyombo vya habari kubainisha hali halisi ya mwenendo wa uchaguzi na Mamlaka itafanyia kazi taarifa zilizoibuliwa ndani ya muda sahihi.
4. Zoezi hili linaendeshwa kwa dhamira ya kukuza mfumo shirikishi katika kujenga mazingira ya uchaguzi huru na haki wa mwaka 2020 na kuimarisha utekelezaji wa misingi ya utawala bora, hususan katika kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi.

**WASHIRIKI WA MASHINDANO**

Mashindano ya wandishi wa habari ya mwaka 2020 yatakuwa wazi ambapo kila mwanahabari atakuwa huru iwe amejiajiri au ameajiriwa katika chombo cha habari au hakuajiriwa katika vyombo hivi. Kinachohitajika aandae kazi yake na itolewe katika chombo cha habari chochote kama vile redio, gazeti, televisheni au mitandao wa kijamii. Sambamba na mahitaji hayo, taarifa hiyo iwasilishwe ZAECA kwa muda sahihi.

**VIGEZO VYA KAZI ZITAKAZO SHINDANIWA**

Kazi itakayoshinda itazingatia vigezo au sifa zifuatazo;

(i) Inatakiwa kuwa ni ya ukweli na sahihi.
(ii) Taarifa inatakiwa kuwa na vyanzo sahihi.
(iii) Taarifa inasisitizwa kuzingatia haki.
(iv) Kazi iandaliwe kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza.
(v) Washiriki wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni za nchi, misingi na maadili ya uandishi wa habari kwa ukamilifu.
(vi) Inasisitizwa taarifa iwe na mchango mzuri katika kuleta mabadiliko kwa jamii.
(vii) Taarifa iwe na awanda mapana ya ushirikishwaji jamii ambayo yatazingatia mambo mbalimbali ikiwemo jinsia, sauti za ndani na

njee ya mjini na vijijini, pamoja na kutoa sauti kwa makundi maalum.

(viii) Matumizi ya mbinu mbali mbali za utafiti zitumike katika kuandaa taarifa.

(ix) Taarifa itoe fursa kwa ZAECA kufuatilia au kuchunguza vitendo vilivyoibuliwa.

**AINA NA IDADI YA KAZI ZITAKAZO SHINDANIWA**

Mashindano haya yatashirikisha kazi za habari na picha zitakazochapishwa na kutangazwa /kurushwa kupitia;

(a) magazeti(b)Televisheni (c)Redio na (d) Mitandao ya kijamii(social new media).

Kila mwandishi anayofursa ya kushiriki katika mashindano haya kwa kuwasilisha kazi **moja(1)** hadi tatu kwa kila aina ya chombo cha habari.

**MUDA WA KUWASILISHA TAARIFA**

Mashindano yataanza tarehe 1/7/2020, taarifa zinazoshindaniwa zinatakiwa ziwasilishwe muda wa kazi katika ofisi za ZAECA kabla ya kuchapishwa au kutolewa hewani. Tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa taarifa kwa mashindano ya 2020 ni siku ya Ijumaa sawa na tarehe 11/5/2021.

**MFUMO WA UWASILISHAJI KAZI**

Kazi zinatakiwa kuwasilishwa kupitia utaratibu ufuataao;

**(a)** Kipindi (program), inasisitizwa kuwasilishwa kabla hakijarushwa hewani na iingizwe kwenye CD ikiwa katika bahasha inayoonesha:-

- Anuani kamili, nambari ya simu na barua pepe (email) ya mwandishi.

- Jina la kipindi

- Jina la chombo kitakachotuma taarifa hiyo.

- Iambatanishwe na muongozo (script) ya kipindi kilichowasilishwa.

- Ikiwa kipindi kilikuwa live (moja kwa moja) CD iwasilishwe, namna kilivyorushwa hewani.

**(b)** Kwa upande wa makala /taarifa zilizochapishwa **Magazetini,** inapendekezwa soft copy ziwasilishwe kabla ya kuchapishwa na baada ya kuchapishwa ikamilishwe kwa kuwasilishwa;

- Sehemu (cutting) halisi iliyotolewa katika gazeti lililochapisha taarifa hiyo

- Iwapo kumetumika "pen name", kuwepo kwa uthibitisho wa kazi ya mshiriki ikiwemo saini au muhuri wa mhariri.

**(c)** Kwa upande wa vipindi (program/ documentary) makala /taarifa zilizotolewa hewani (ON AIR) kwenye **Telivisheni na Radio,** inapendekezwa nakla /CD zake ziwasilishwe kabla ya kurushwa hewani na baada ya kwenda hewani ikamilishwe kwa kuwasilishwa;

- Anuani kamili, nambari ya simu na barua pepe (email) ya mwandishi

- Jina la kipindi

- Jina la chombo kilichotumika kurusha taarifa hiyo.

- Iambatanishwe na muongozo (script) wa kipindi husika.

- Ikiwa kipindi kilikuwa live (moja kwa moja) CD ya kipindi iwasilishwe namna ilivyorushwa hewani.

**(d)** Kwa upande wa **Mitandao ya kijamii** 'social media' kama vile tovuti, blogi, online TV, na nyenginezo kazi zitiwe kwenye CD na zioneshe taarifa kama inavyoonekana katika (a) hapo juu kwenye sehemu hii. Pia ibainishe 'link' ambayo inaweza kufuatiliwa na kupatikana taarifa hiyo kupitia mtandaoni.

Inapendekezwa nakla /CD zake ziwasilishwe kwa "soft copy" kabla ya kurushwa hewani na baada ya kwenda hewani ikamilishwe kwa kuwasilishwa;

- Anuani kamili,nambari ya simu na barua pepe (email) ya muandaaji.

- Jina la kipindi

- Jina la chombo kilichotumika kurusha taarifa hiyo.

- Iambatanishwe na muongozo (script) ya kipindi husika.

**UPOKEAJI WA KAZI**

Kazi zitapokelewa siku na wakati wa saa za kazi. Mshiriki aliyekuwepo Unguja anatakiwa awasilishe kazi yake katika Ofisi za ZAECA Makao Makuu, Victoria garden- Mnazimmoja na aiwasilishe Kitengo cha Uhusiano.

Washiriki walioko Mkoa wa Kusini Pemba wanatakiwa kuziwasilisha kazi zao katika Ofisi za ZAECA jengo la Zan Air ghorofa ya 3 mkabala na maduka ya Bakhressa Chakechake.

Washiriki wa walio Mkoa wa Kaskazini Pemba, wanatakiwa kuwasilisha kazi zao katika Ofisi ya ZAECA iliyopo Majengo ya MECCO, Kinyasini, Wete Pemba.

Kazi ya mshiriki itakayopokelewa ZAECA itarikodiwa katika daftari maalum. Baada ya kupokelewa mshiriki ahakikishe ameorodhesha jina, mawasiliano na saini yake kabla ya kuondoka, ni lazima kufanya hivyo.

**N.B. INASISITIZWA KAZI KUPELEKWA OFISI ZA ZAECA KABLA YA KUTOLEWA KWENYE VYOMBO ILI KUWARAHISISISHIA MAAFISA WA ZAECA KUFANYA UTUATILIAJI KWA MUDA SAHIHI.**

***Kwa mawasiliano Zaidi unaweza kuwasiliana na ZAECA kupitia anuwani zifuatazo;***

***P.O.BOX 3650, Victoria Garden – Mnazimmoja, Zanzibar***

***Simu Makao Makuu (Unguja) 0774824242,***

***Kaskazini Pemba 0738 311 338/ 0623 799 629, au***

***Kusini Pemba +255 24 245 2521/ 0776651112***

***Email: info@zaeca.go.tz***

***Website: www.zaeca.go.tz***

**Imetolewana**

**@ Kitengo cha uhusiano**

**Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA).**